

Ethical Trading Initiative

# Kuunda maeneo salama na yenye heshima ya kazi kwa kila mtu



- ✅ **Kila mtu**, ikiwemo wewe, ana haki ya kutendewa kama binadamu (kwa heshima), bila kujali kazi anayofanya na kwa haki.
- ✅ **Kila mtu**, ikiwemo wewe, anatarajiwa kuwatendea wengine kwa heshima, haki na hadhi ileile.
- ❌ **Hakuna mtu** anayepaswa kufanyiwa ukatili au unyanyasaji kwa sababu ya jinsia yake anapokuwa kazini. Hii inajumuisha, unapokuwa mahali pa kazi, shambani, kwenye boti au meli; unapokuwa kwenye safari ya kikazi, unaposafiri kwenda na kutoka mahali pa kazi; na ikiwa unakaa kwenye makazi ambayo mwajiri wako hutoa.



# Dhuluma ya kijinsia na unyanyasaji (GBVH) ni ukatili au unyanyasaji kulingana na jinsia ya mtu. Hii ni pamoja na ukatili au vitisho vya ukatili.

Unyanyasaji ni mwenendo wa kimwili, wa maneno au usio wa maneno, ambao unamfanya mtu ahisi wasiwasi, kutishwa, kukerwa au kudhalilishwa kazini. Hii pia ni pamoja na ukatili au unyanyasaji unaoelekezwa hasa kwa watu wa jinsia mahususi.

- Mifano ya tabia isiyokubalika hapa ni kutukana kwa kutumia lugha ya kingono, kumtania au kumkejeli mtu kwa sababu ya jinsia yake.
- Mifano ya tabia mbaya zaidi ni kuomba miadi ya kimapenzi au ngono kwa kubadilishana na kazi, kufanya upya mikataba au kazi rahisi, iwe wakati wa kuandikishwa au kuajiriwa na unyanyasaji wa kingono.

**Mifano mingine ni pamoja na:**

# Kuzuia:
## Kila mtu ana jukumu la kutekeleza

| Mwajiri wako na mahali pako pa kazi |
| --- |
| Ana jukumu la kukuandalia wewe na wafanyakazi wenzako eneo na njia salama ya kufanya kazi |
| Anapaswa kuzungumza na wewe pamoja na wafanyakazi wenzako kuhusu dhuluma ya kijinsia na unyanyasaji (GBVH): jinsi inavyotokea, wakati gani, wapi na kwa nini. Anapaswa kushughulikia njia za kuzuia jambo hili pamoja nawe au mfanyakazi anayewakilisha/anayeweza kuzungumza kwa niaba ya wafanyakazi. |
| Anapaswa kuelezea jinsi anavyotarajia ufanye kazi yako, ikiwemo kile kinachokubalika na kisichokubalika. Mwajiri wako anapaswa kuelezea matokeo yatakayotokea ikiwa mtu hatatii kanuni hizi. |
| Anapaswa kukufundisha kuhusu kile unachopaswa kufanya ikiwa utaona au kusikia kitu ambacho si sahihi.  Anapaswa kukuambia jinsi unavyoweza kuripoti wasiwasi wako na kwa nani. |



## Wewe na wafanyakazi wengine

- Mna haki ya kujihisi salama na kustareheka kazini.
- Mna haki ya kuuliza ikiwa kuna jambo lolote ambalo haliko wazi kwenu. Ni sawa kuuliza maswali.
- Mna haki ya kukusanyika pamoja na wafanyakazi wengine na kuwakilisha wasiwasi wenu wa pamoja na kujadiliana na waajiri wenu ili kupata masharti na mazingira bora ya kazi kama sehemu ya chama cha wafanyakazi.
- Mnaweza kuzungumza na mtu anayeaminika, ikiwa mtu atasema au kufanya kitu ambacho hakionekani kuwa sahihi.



# Kuripoti:
## Ikiwa kuna jambo linalokusumbua, unaweza kuzungumza na mtu

- Ni sawa iwapo huna uhakika ikiwa jambo fulani ni dhuluma ya kijinsia na unyanyasaji (GBVH). Ikiwa kuna jambo limekutokea au ikiwa una wasiwasi kuhusu mtu mwingine, unaweza kuzungumza na mtu unayemwamini wakati wowote.
- Unaweza kuripoti bila kujitambulisha (si lazima utaje jina lako) au kwa siri (ni watu wale tu ambao unahitaji wajue ndio watakaojua).
- Mtu anayekusaidia ataelezea mchakato wa kuripoti wasiwasi wako, hatua kwa hatua. Ni sawa kuuliza maswali. Ni sawa kuomba taarifa zaidi.
- Unaweza kuwa na mtu anayekusaidia, kama vile rafiki, mwakilishi wa chama cha wafanyakazi au mwanafamilia.
- Ripoti yako inapaswa kuchukuliwa kwa uzito. Mwajiri wako atachukua hatua ili kuelewa kilichotokea.













# Urekebishaji:
## Kurekebisha mambo

- Unapaswa kuulizwa kuhusu kile kitakachoboresha mambo. Hii inaweza kuwa hatua mbalimbali, ikiwemo kuomba msamaha au mabadiliko katika kazi yako.
- Ikiwa mtu amefanya jambo lisilokubalika, anapaswa kukabiliana na matokeo ya haki.
- Ikiwa mabadiliko mahali pa kazi yanahitajika, mwajiri wako anapaswa kuonyesha jinsi mafunzo yamepatikana na jinsi dhuluma ya kijinsia na unyanyasaji (GBVH) ya siku zijazo inavyozuiwa

**Ikiwa una maswali kuhusu jambo hili au unahitaji kuzungumza na mtu, unaweza kuwasiliana na mwakilishi wa mahali pako pa kazi, meneja unayemwamini na:**

Ethical Trading Initiative

ETI is a leading alliance of NGOs, trade unions, and companies advancing human rights in supply chains. Our vision is of a world of work that protects human rights, ensures dignity for all, provides opportunity and is free of exploitation and abuse.